# MwanaHisa

CRDB BANK PLC

Toleo La Machi, 2018




# Yaliyomo

2 | Benki yapata faida ya shilingi bilioni 69 mwaka 2017

3-4 | Ufunguzi wa Tawi la Benki ya CRDB LAPF Dodoma wafana

5 | Wajue wajumbe wapya wa Bodi ya Benki ya CRDB

6 | Matukio katika picha

7 | Tangazo la malipo ya malimbikizo ya gawio

7 | Karibu kwenye Mkutano Mkuu wa 23 wa Wanahisa

8 | Kibonzo – (Umuhimu wa kutunza Cheti cha Hisa)

@crdbbank

@CRDBBankPlc

crdbbankplc

CRDB Bank Plc

## ANUANI

Mhariri Mwanahisa

CRDB Bank Plc
Office Accommodation Scheme
Mtaa wa Azikiwe, Ghorofa ya 4
S. L. P. 268, Dar-es-Salaam
Simu Na. 022 - 2114237, 022-21174421 - 7
Fax na. 022 - 2131005
investorrelations@crdbbank.com au
shareholders@crdbbank.com
www.crdbbank.com

## *Maoni kutoka kwa mwanahisa*

Wanahisa wanapewa fursa ya kufikisha maoni, ujumbe au mapendekezo katika jarida hili kwa kutumia anuani inayoonekana hapo juu.

# Benki yapata faida ya shilingi bilioni 69 mwaka 2017

***Benki ya CRDB na Kampuni zake Tanzu zimepata faida baada ya kodi ya shilingi bilioni 69 mwaka 2017 licha ya changamoto zilizoikabili sekta ya kifedha ikiwemo hali ngumu ya ukwasi. Faida iliyopatikana mwaka 2017 ilipungua kwa asilimia 7 ikilinganishwa na faida ya shilingi bilioni 74 iliyopatikana mwaka 2016.***

Rasilimali za Benki na Kampuni zake Tanzu ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 5,416 mwaka 2016 hadi shilingi bilioni 5,924 mwaka 2017. Amana pia ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 4,110 mwaka 2016 hadi shilingi bilioni 4,236 mwaka husika. Mikopo iliyodorora ilipungua kutoka asilimia 14.0 (ya mikopo yote) mwaka 2016 hadi asilimia 13.4 mwaka 2017. Pato kwenye mtaji lilipungua kutoka asilimia 10.3 mwaka 2016 hadi asilimia 9.2 mwaka husika.

***Matokeo ya viashiria mbalimbali vya utendaji (wa Benki ya CRDB na Kampuni zake Tanzu) kwa Mwaka 2017 ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:***

| VIASHIRIA VYA UTENDAJI | JAN — DESEMBA 2016 *(shilingi bilioni)* | JAN - DESEMBA 2017 *(shilingi bilioni)* | KUONGEZEKA/KUPUNGUA *(kwa asilimia)* |
|---|---|---|---|
| Rasilimali | 5,416 | 5,924 | 9 ▲ |
| Amana | 4,110 | 4,236 | 3 ▲ |
| Faida baada ya kodi | 74 | 69 | 7 ▼ |
| Pato kwenye rasilimali (ROA) | 2.2% | 1.8% | 0.4 ▼ |
| Pato kwenye Mtaji (ROE) | 10.3% | 9.2% | 1.1 ▼ |

Mchango wa kampuni tanzu umeendelea kuongezeka kwani kampuni zote zilipata faida katika kipindi hiki.

Kampuni Tanzu ya CRDB Microfinance Services Company Limited ilipata faida baada ya kodi ya shilingi milioni 800 na Kampuni Tanzu ya Benki ya CRDB Burundi ilipata faida baada ya kodi ya shilingi bilioni 3.2 . Kampuni ya CRDB Insurance Broker, ilipata faida ya shilingi milioni 1,049.

Benki ya CRDB imeendelea kuwa imara kwenye soko kwa kushikilia takriban asilimia 21 ya jumla ya amana na rasilimali katika sekta ya benki, ambayo imeifanya ishike nafasi ya kwanza kwa ukubwa wa mizania nchini Tanzania.

Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB ilichukua hatua kadhaa ili kuimarisha utekelezaji wa mkakati wa biashara kwa mwaka 2017. Mojawapo ya hatua hizo ilikuwa ni kudhibiti ukuaji wa gharama za uendeshaji kwa kupunguza kasi ya kupanua mtandao wa Benki na kuboresha matumizi ya rasilimali ili kuongeza tija.



# Rais Magufuli afungua tawi jipya la Benki ya CRDB mkoani Dodoma

*Benki ya CRDB imeendelea kupanua wigo wa kuwahudumia wateja wake kwa kufungua tawi jipya katika jengo la LAPF Mkoani Dodoma, ambapo mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli. Akizungumza katika hafla hiyo, Mheshimiwa Rais aliipongeza Benki ya CRDB kwa kupanua wigo wa huduma zake mkoani Dodoma ili kuendana na kasi ya ukuaji wa makao makuu ya nchi.*

“***Nimefurahi sana kuona Benki ya CRDB inaunga mkono mkakati wa Serikali kuhamishia shughuli zake hapa Dodoma. Ni matumaini yangu kuwa tawi hili litaboresha upatikanaji wa huduma za kibenki hapa Dodoma na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo ya mkoa na nchi yetu kwa ujumla,***” alisema Mheshimiwa Rais.

Rais Magufuli alitumia fursa hiyo kutoa wito kwa wananchi wote wa mkoa wa Dodoma, kutumia fursa ya ufunguzi wa tawi hilo jipya kwa kuendeleza na kuboresha shughuli zao za maendeleo. Aliwasihi wananchi kutoogopa kutumia fursa zinazotolewa na mabenki katika kupata mikopo pamoja na ushauri wa masuala mbalimbali ya kifedha.

Dkt. Magufuli aliipongeza Benki ya CRDB kwa kutoa kipaumbele katika kuiwezesha sekta ya viwanda hapa nchini. Serikali kwa upande wake imejipanga vizuri ili kuhakisha Tanzania inafikia malengo ya kuwa nchi yenye uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

“***Dkt. Kimei ameeleza hapa ni kwa jinsi gani Benki ya CRDB imekuwa ikiweka sera na mikakati inayotoa kipaumbele kwa sekta za viwanda na kilimo ambazo ni muhimu sana katika kuhahikisha tunakuwa na malighafi za kutosha na zenye ubora kwa ajili ya viwanda vyetu, niwapongeze sana kwa hili***” alisema Dkt. Magufuli.

Mheshimiwa Rais pia aliyataka mabenki nchini kupunguza riba katika mikopo wanayotoa. Alisema kuwa riba kubwa imekuwa changamoto inayochangia wateja wengi kushindwa kurejesha mikopo na wengine kuogopa kukopa kabisa.

Dkt. Magufuli alipongeza Benki ya CRDB kwa kubuni njia mbali mbali mbadala za kutolea huduma hususani SimBanking, FahariHuduma Wakala na Internet banking ambazo zimekuwa msaada mkubwa katika kufikisha huduma za kibenki kwa wananchi walio wengi, ambao kwa muda mrefu wamekuwa nje ya mfumo rasmi wa kibenki.

"Ninaposema mabenki yasambaze huduma mpaka vijijini simaanishi mfungue matawi kama haya, ila nawataka mbuni njia mbadala za kuwafikia wateja kama kuingia ubia na mawakala 'Agent banking', huduma za SimBanking na Internet Banking kama Benki ya CRDB mlivyotanikiwa kutanya, niwapongeze sana," alisema Dkt. Magufuli.

Vilevile mheshimiwa Rais alipongeza Benki ya CRDB kwa kuendelea kuwa Benki imara na kusisitiza kuwa kama taasisi zote za Serikali zilizobinatsishwa zingeiga mtano wa Benki ya CRDB taifa lingepiga hatua kubwa sana kimaendeleo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB Bw. Ally Hussein Laay alisema mbali ya kutungua tawi hilo, Benki ya CRDB imeshapata eneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi kubwa zaidi itakayo kuwa sehemu ya makao makuu ya Benki hiyo. Pamoja na hayo Bw. Laay alimhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa Benki ya CRDB itaendelea kuweka mikakati endelevu na yenye manufaa kwa wateja na watanzania kwa ujumla.

***"Azma yetu kuu ni kuifanya benki ya CRDB kuwa benki chaguo namba moja la watanzania wote yaani "First choice bank". Azma hii inatufanya kuendelea kuwa wabunifu zaidi na kuendelea kusimamia misingi yetu ya kuwa benki ya kizalendo yenye mtazamo wa kimataifa,"*** alisema Bw. Laay.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Dkt. Charles Kimei alisema kuwa mahitaji ya huduma za kibenki katika jiji la Dodoma yamekua kwa kasi hasa baada ya Serikali kuhamia katika mkoa huo na hivyo kuhamasisha Benki kupanua wigo wake ili kukidhi mahitaji ya huduma za kibenki.
"Tumechukua uamuzi huu ili kuendana na kasi ya serikali yako ya kuhamishia rasmi makao makuu hapa Dodoma. Ni dhahiri kuwa kitendo cha serikali kuhamia rasmi hapa Dodoma kitaongeza idadi ya watu na hivyo kuongeza maradatu mahitaji ya huduma za kibenki" alisema Dkt. Kimei.

Dkt. Kimei alisema mkoa wa Dodoma ni kati ya mikoa ambayo Benki ya CRDB ina matawi mengi. Benki hiyo ina jumla ya matawi 9 mkoani humo ambayo ni Dodoma, UDOM, Chamwino, Bunge, Gairo, Kondoa, Mpwapwa, Miuji na Kibaigwa. Dkt. Kimei alisema Benki ya CRDB inashiriki na kuchangia kwa kiwango kikubwa ukuaji wa uchumi wa nchi kupitia ulipaji kodi, ajira, huduma za kijamii na utoaji mikopo.

***"Mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka jana, Benki ya CRDB ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 3.3 kwenye sekta za kilimo, uchukuzi, utalii, viwanda na ujenzi wa miundombinu"*** alisema Dkt. Kimei.

Katika hafla hiyo, Benki ya CRDB pia ilimkabidhi Mheshimiwa Rais hundi ya kiasi cha shilingi milioni 100 ikiwa sehemu ya wajibu wa Benki hiyo kusaidia jamii inayoizunguka (Corporate Social Responsibility). Akizungumza wakati wa makabidhiano, Dkt. Kimei alisema Benki ya CRDB inatambua kuwa serikali peke yake haiwezi kutatua kila changamoto katika jamii hivyo Benki hiyo kama mdau mkubwa wa maendeleo ina jukumu la kuisaidia serikali kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii.

Mheshimiwa Rais aliishukuru Benki ya CRDB kwa kuwa mdau mkubwa wa kuchangia maendeleo, huku akizitaka taasisi nyingine kuiga mfano wa Benki ya CRDB katika kuisaidia jamii inayoizunguka. Akizungumza wakati akikabidhi msaada huo uliotolewa na Benki ya CRDB kwa mkuu wa mkoa wa Dodoma Dkt. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Rais aliagiza fedha hizo zitumike katika ujenzi wa wodi ya wagonjwa hospitali ya mkoa wa Dodoma.

"Naelekeza fedha hizi zitumike kujenga wodi ya wagonjwa katika hospitali yetu ya mkoa, nitakuja mwenyewe kuhakikisha zimetumika vizuri. Nitauomba uongozi wa Benki ya CRDB uungane na mimi katika uzinduzi wa wodi hii ambayo tutaipa jina la 'Wodi ya Benki ya CRDB' ", alisema Mheshimiwa Rais.

# Wajue wajumbe wapya wa Bodi ya Benki ya CRDB.

*Hivi karibuni Benki Kuu ya Tanzania imeidhinisha wajumbe watatu wapya wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB ambao wanakamilisha safu ya wajumbe 12. Wajumbe hao ni Dkt. Neema Munisi Mori, Bw. Charles Edward Kichere na Bw. Jes Klausby.*

*Dkt. Mori alichaguliwa wakati wa Mkutano Mkuu wa 22 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB uliofanyika jijini Arusha mwezi Mei, 2017 akiwakilisha kundi la wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja. Bw. Kichere na Bw. Klausby wameteuliwa na DIF kuwakilisha wanahisa wenye hisa zaidi ya asilimia 10 ya hisa za Benki. Bw. Kichere ameteuliwa kujaza nafasi iliyoachwa wazi na Bw. Bede Philip Lyimo aliestaafu na Bw. Klausby ameteuliwa kuchukua nafasi ya Bw. Kai Kristoffersen ambae pia amestaafu.*

## Wasifu wa wajumbe wapya wa Bodi




***Dkt. Neema Munisi Mori*** ni Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Fedha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania na Mjumbe wa Bodi ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na Taasisi ya Utoaji Mikopo nchini- EFL. Dkt. Mori ana Shahada ya Uzamivu katika masuala ya Biashara ya Kimataita (akijikita zaidi katika Utawala wa Kampuni) ya Chuo Kikuu cha Agder, Norway, Shahada ya Uzamili ya Uongozi wa Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam nchini Tanzania na Shahada ya Kwanza katika masuala ya Fedha ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.



***Bw. Jes Klausby*** ni Mshauri Mwandamizi wa masuala ya Uchambuzi wa Kibenki, Benki Kuu ya Denmark. Aliwahi kuwa Mwenyekiti na Mjumbe wa Bodi ya Dansk Pantebrevsbors na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Nykredit. Ana Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika masuala ya Hesabu na Uchumi ya Chuo Kikuu cha Aarhus, Denmark.



***Bw. Charles Edward Kichere*** ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato nchini Tanzania (Tanzania Revenue Authority - TRA). Ana Shahada ya Kwanza ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini jijini Dar es Salaam, Tanzania, Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara katika masuala ya fedha (MBA) -Finance ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Stashahada ya Usimamizi wa Fedha za Miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo kutoka Africa Renaissance Centre, Mbabane Swaziland, Shahada ya Kwanza ya Biashara katika Uhasibu (B.Com Accounting) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

# Ufunguzi wa tawi la Benki ya CRDB mkoani DODOMA




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Dkt. Charles Kimei.*



*Viongozi na wafanyakazi wa Benki ya CRDB pamoja na wageni waalikwa wakifuatilia ufunguzi wa tawi la Benki ya CRDB mkoani Dodoma*




*Rais Magufuli akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali na wajumbe wa Bodi na Menejimenti ya Benki ya CRDB*




*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB Bw. Ally Laay na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo Dkt. Charles Kimei wakimkabidhi Rais Magufuli mfano wa hundi ya shillingi milioni 100 kuchangia huduma za jamii. Kiasi hicho cha fedha kitatumika katika ujenzi wa wodi ya wagonjwa hospitali ya mkoa wa Dodoma*

# Malipo ya gawio kwa wanahisa ambao hawajachukua gawio kwa muda mrefu

Benki ya CRDB inawatangazia wanahisa wote ambao hawajachukua gawio kwa muda mrefu kufika katika tawi lolote la Benki ya CRDB kwa ajili ya kuhakiki taarifa zao na kufanya taratibu za malipo.

Mwanahisa atatakiwa kutekeleza yafuatayo ili kulipwa gawio lake:

A. Kujaza fomu ya kuboresha kumbukumbu za mwanahisa zinazopatikana kwenye matawi ya Benki na kuituma kwa Katibu au Tawi lolote la Benki ya CRDB lililo karibu naye.

B. Wanahisa wasio na akaunti katika Benki yoyote ile, wanashauriwa kufungua Akaunti ya Busara ambayo imeanzishwa kwa ajili ya wanahisa kupitia tawi lolote la Benki ya CRDB.

C. Fomu iliyojazwa irudishwe Benki ikiwa imeambatishwa na nakala ya cheti cha hisa (CDS Receipt) pamoja na barua ya maombi ya kulipwa gawio.

# Karibu kwenye semina na Mkutano Mkuu wa 23 wa Benki ya CRDB

Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Menejimenti ya Benki ya CRDB inachukua fursa hii kuwaalika wanahisa wote wa Benki kuhudhuria Mkutano Mkuu wa 23 wa Benki ya CRDB utakaofanyika siku ya Jumamosi tarehe 19 Mei 2018, katika ukumbi wa Simba uliopo Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (AICC) jijini Arusha kuanzia saa 3 kamili asubuhi. Mkutano Mkuu utatanguliwa na semina ya wanahisa itakayofanyika siku ya Ijumaa tarehe 18 Mei, 2018 katika ukumbi wa Simba katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (AICC) jijini Arusha kuanzia saa 3 kamili asubuhi.

Mkutano Mkuu hufanyika kila mwaka ili kuwawezesha wanahisa kujua maendeleo ya benki yao na kushiriki kutoa maoni na kupitisha maamuzi muhimu kwa ajili ya kuongeza tija na kuboresha utendaji .

Mkutano Mkuu ni fursa muhimu sana kwani hutoa nafasi kwa wanahisa kuwasilisha mapendekezo yao na kuuliza maswali mbalimbali na kupata majibu moja kwa moja kutoka kwa uongozi wa Benki. Kila mwanahisa ana haki ya kushiriki Mkutano Mkuu.

Wanahisa watakaoshindwa kushiriki au kufika kwenye Mkutano Mkuu wanashauriwa kutokupoteza fursa hiyo kwa kuchagua mwakilishi ambaye atahudhuria mkutano mkuu kwa niaba yao. Ili kufanya hivyo, mwanahisa anatakiwa kujaza fomu ya uwakilishi (proxy form) na kuiwasilisha kwa Meneja wa Tawi lolote la Benki lililopo karibu naye. Pia mwanahisa anaweza kuandika maoni yake na kumkabidhi mwakilishi atakaye mchagua.

**Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana nasi kwa anuani/simu ifuatayo:**

@crdbbank

@CRDBBankPlc

crdbbankplc


CRDB Bank Plc

Katibu
CRDB Bank Plc
Office Accommodation Scheme
Mtaa wa Azikiwe. Ghorofa ya 4
S. L. P. 268, Dar-es-Salaam
Simu Na. 022 - 2114237, 2117442 - 7
Fax na. 022 - 2131005
Barua pepe: *John.Rugambo@crdbbank.com au shareholders@crdbbank.com*
Au Meneja wa Tawi la Benki ya CRDB lililo karibu nawe

CRDB BANK
The bank that listens

# MAMA FAIDA NA BABA MTAJI

## WAKIZUNGUMZIA UMUHIMU WA KUTUNZA CHETI CHA HISA




Babatau cartoons 2016



CRDB BANK
The bank that listens